



*Makao Makuu ya TBS*

## MAABARA

TBS ina maabara saba zenye vifaa vya kisasa na wataalamu wa kutosha. Maabara hizo ni: -

- Maabara ya Kemia
- Maabara ya Uhandisi Umeme
- Maabara ya Uhandisi Mitambo
- Maabara ya Uhandisi Ujenzi
- Maabara ya Chakula
- Maabara ya Ngozi, Nguo na Kondomu
- Maabara ya Ugezi

## KITUO CHA TEKNOLOJIA YA UFUNGASHAJI

TBS pia inacho Kituo cha Teknolojia ya Ufungashaji (PTC) kilichoanzishwa mahususi kwa malengo makuu matatu: -

- Kusaidia na kuratibu maendeleo ya tasnia ya ufungashaji;
- Kutoa mafunzo kwa wazalishaji kuhusiana na teknolojia ya ufungashaji;
- Kudhibiti ubora wa nyenzo za kufungashia ikiwa ni pamoja na kutoa yeti vya ubora kwa nyenzo za kufungashia zilizotengenezwa kwa kuzingatia viwango vya Tanzania;
- Kutoa huduma ya upimaji wa nyenzo za kufungashia.



**Kwa maelezo zaidi tuandikie kwa kutumia anwani hii:**

Shirika la Viwango Tanzania  
S I P 9524 Dar es Salaam  
Tanzania

Simu: 255 22 2450206/2450949

Faksi: 255 22 2450959

Baruapepe: info@tbstz.org

Tovuti: www.tbstz.org

Au tuone katika eneo la **URBUNGO**, Dar es Salaam  
kwenye makutano ya Barabara za  
Morogoro na Sam Nujoma.



**SHIRIKA LA VIWANGO  
TANZANIA (TBS)**

**KWA UFUPI**

*Baadhi ya mameneja na maojisa wa TBS wakiwa katika  
banda la TBS wakati wa maonyesho ya utunishi.*

**SHIRIKA LA VIWANGO TANZANIA (TBS)**





*Maalumu akiwanesha Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji ya Bunge jinsi upinjaji unavyofanyika katika Maabara ya Chakula*



*Maalumu akiangalia umara wa kondomu katika Maabara ya Kondomu.*



*Maofisa wa TBS wakiangalia ubora wa bidhaa sokoni. TBS hufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa kushukika katika masoko na maduka mbalimbali.*

Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ni Shirika la Umma chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, lililoundwa chini ya Sheria ya Bunge Nambari 3 ya mwaka 1975 na kurekebishwa chini ya Sheria Nambari 1 ya mwaka 1977.

## MAJUKUMU YA TBS

### **TBS ina majukumu makuu manne:**

- Kuweka na kusimamia viwango vyote vya kitaifa; Kutoa ushauri viwandani juu ya uzalishaji wa bidhaa bora;
- Kupima na kuhakikisha vipimo vinavyotumika viwandani;
- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa viwandani
- Kuelimisha umma juu ya masuala yote yanayohusu uwekaji na usimamiji wa viwango pamoja na udhibiti wa ubora wa bidhaa viwandani.
- Utoaji wa leseni na yeti vya ubora wa bidhaa zinazozalishwa ndani na nje ya nchi

## VIWANGO VYA TANZANIA

Viwango vya Tanzania ni viwango vya kitaifa vilivyokwishawekwa au vitakayowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Viwango Na. 3 ya mwaka 1975 vikielezea kanuni za uzalishaji, uhifadhi na ufungashaji wa bidhaa bora.

Mpaka sasa TBS imeishaandika viwango zaidi ya 1000 katika nyanja za Kilimo na Chakula, Ngozi, Madawa, Nguo, Uhandisi mirambo, Uhandisi ujenzi na Uhandisi umeme.

## UTEKELEZAJI WA VIWANGO

Viwanda kadhaa hapa nchini, vya serikali pamoja na vya watu binafsi, hufuata na kutumia viwango vya kitaifa katika uzalishaji na uuzaji wa bidhaa mbalimbali nchi za nje.

Ili wananchi waweze kufaidika na viwango, TBS inaendesha mpango wa utibiti wa ubora wa bidhaa, ambao unaliwezesha Shirika kutoa leseni kwa wazalishaji bidhaa wanaothibitishwa kuwa wanazalisha kulingana na kiwango cha kitaifa cha bidhaa husika ambayo huwaruhusu kutumia alama ya ‘tbs’ ya ubora wa bidhaa.

## FAIDA ZA VIWANGO

- Huweka usawa katika uwanja wa biashara;
- Huondoa mkanganyiko kuhusiana na bidhaa;
- Husaidia kufungua masoko zaidi;
- Hurahisisha biashara baina ya nchi na nchi;
- Hutoa uhakikisho wa ubora, usalama, kuaminiwa na ufanisi;

## FAIDA ZA ALAMA YA UBORA YA ‘tbs’



TZS .....

### **Kwa mteja/mlaji**

- Humthibitishia kuwa bidhaa husika inafaa kwa matumizi husika;
- Huwezesha kupungua kwa bei ya bidhaa kutokana na ushindani;
- Humhakikishia usalama wake kiafya na katika matumizi;
- Huongeza ubora wa maisha;
- Hulinda mazingira yake.

### **Kwa mzalishaji**

- Humpa uwezo mkubwa zaidi wa kushindana sokoni;
- Humpatia wateja zaidi;
- Humwondolea usumbufu wa kupima bidhaa kwa kuzingatia matakwa ya mnuuzi;
- Humkinga dhidi ya ushindani na bidhaa duni zisizo na viwango.